Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO , NO. 8, JULAI 2023

TUNABORESHA AFYA
MTU NI AFYA • AFYA NI MTAJI



# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, AFYA NI MTAJI

# TAHARIRI

Kwa niaba ya Uongozi, Menejimenti na Watumishi wote wa Wizara ya Afya napenda kukukaribisha ndugu msomaji wa jarida hili lililosheheni habari za matukio muhimu ya Wizara ya Afya na Sekta ya Afya kwa ujumla wake.


Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kutoa rasilimali fedha na kuboresha zaidi Sekta ya Afya nchini ambapo tumeshuhudia kuongezeka bajeti ya Wizara ya Afya kutoka Shilingi Trilioni 1.1 mwaka 2022/2023 hadi Shilingi Trilioni 1.2 mwaka 2023/2024.

Kipekee napenda kulishukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitisha makadirio ya Bajeti ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2023/2024 ya Shilingi Trilioni 1.2 kwa asilimia mia moja.

Mambo mengi mazuri yamefanyika kupitia uongozi mahiri wa viongozi wetu wakiongozwa na Waziri wetu Mhe. Ummy Mwalimu pamoja na Msaidizi wake Mhe. Godwin Mollel Naibu Waziri wa Afya.

Sisi tukiwa watendaji ndani ya Wizara tutaendelea kuhakikisha tunakuwa wabunifu, kufanya kazi kwa juhudi ili kuhakikisha azma ya Serikali yetu pendwa inatekelezwa kikamilifu kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya.

**Dkt. Seif Shekalaghe**
**KATIBU MKUU, WIZARA YA AFYA.**



Skani kwa kutumia kamera ya Simu yako kupakua kidigitali Jarida hili.




**BODI YA UHARIRI**

**MWENYEKITI**
Englibert Kayombo

**WAJUMBE**
Catherine Sungura
Emmanuel Malegi
Majid Abdulkarim
Said Nyaoza
Hassan Kimweri

**WAHARIRI WA HABARI**
Catherine Sungura
Emmanuel Malegi

**MSANIFU**
Englibert Kayombo

@wizara_afyatz
www.moh.go.tz

# YALIYOMO

**Makamu wa Rais Dkt. Mpango azindua huduma za M-MAMA Hospitali ya Mount Meru, Arusha... UK 1**





**Tanzania ni Salama, Kagera ni Salama, Hakuna tena Ugonjwa wa Marburg...UK 2**

**Rais Samia anazidi kuifungua nchi,Mataifa zaidi ya 120 wakutana Arusha kujadili masuala ya afya ...UK 4**





**Serikali yakabidhi magari kwa ajili ya shughuli za usafi wa mazingira... UK 5**

**Walimu, Wazazi na Jamii wahimizwa kuwahamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi... UK 6**



**Waziri Ummy Mwalimu azindua Baraza jipya la Madaktari... UK 8**





**Shilingi Bilioni 5 zimetengwa kugharamia huduma za upasuaji na matibabu ya kibingwa... UK 19**



Watoto 20 wenye Sikoseli kupandikizwa Uloto bila malipo... UK 21



Serikali yatoa Shilingi Bilioni 3.6 kuboresha miundombinu JKCI... UK 22



Wanafunzi 150 wa Udaktari kutoka Sudan wahamishi- wa Muhimbili... UK 24



Zaidi ya Shilingi Bilioni 5.4 zimetengwa kwa ajili ya vifaatiba katika Hospitali ya Meta, Mbeya... UK 26



Wananchi watakiwa kuzinga- tia mtindo bora wa maisha... UK 27



Kamati ya Bunge yampongeza Rais Dkt. Samia kwa kubore- sha Sekta ya Afya... UK 28



Mfumo wa M- Mama wazinduliwa Hospitali ya Sekoutoure, Mwanza... UK 31



MOI watoa mafuzo ya kwa wataalam katika Hospi- tali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga... UK 32



Upasuaji wa kwanza wa ukarabati wa mrija wa mkojo wafanyika Hospitali ya Ligula Mtwara...UK 32



Serikali yatoa Bilioni 7.3 ujenzi wa majengo ya kutolea huduma za upasuaji, Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Mbeya... UK 34



Mazoezi kwa afya...UK 12

# Makamu wa Rais Dkt. Mpango azindua huduma za M-MAMA Hospitali ya Mount Meru, Arusha.



Na Rayson Mwaisemba
Arusha.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango Juni 22, 2023 azindua huduma ya mfumo wa rufaa na usafirishaji wa dharura kwa mama mjamzito, aliejifungua na mtoto mchanga katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha ikiwa ni kati ya Mikoa 16 inayotoa huduma hiyo nchini Tanzania.

Akizungumza katika hafla hiyo, alieleza kuwa Tanzania inatekeleza mkakati wa kuboresha Afya ya uzazi, mama na mtoto na lishe ambapo una lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi hadi kufikia mia moja kati ya vizazi hai laki moja na vifo vya watoto wachanga vibakie kumi na sita kati ya vizazi hai elfu moja itakapofika mwaka 2025. Ametaja kuwa mojawapo ya changamoto zinazosababisha vifo vya watoto wachanga ni kuchelewa kufika kwenye vituo vya kutolea huduma na kupata huduma stahiki hasa maeneo ya vijijini.

Mfumo huu wa M- mama tangu umeanzishwa hapa Mkoani Arusha Aprili 2023 mpaka Juni 20, 2023 tayari umeshasafirisha jumla ya dharura 607 kati ya hizo asilimia 82 zilikuwa dharura za wakina mama na asilimia 18 zilikuwa dharura za watoto wachanga aidha asilimia 93.7 za wagonjwa wote waliosafirishwa yalitumika magari ya wagonjwa ya serikali na hakukuwa na rufaa kwenye ngazi ya jamii.

Vilevile Serikali itaendelea kuajiri wahudumu wa Afya na ilipeleka wataalamu 100 katika vituo zaidi 40 ili kuwajengea uwezo watoa huduma za Afya kutoa huduma zenye ubora unaostahili na mpango huu utakuwa endelevu ili kuhakikisha inawafikia watoa huduma wengi zaidi na kuhakikisha wakina mama na watoto wanapata huduma bora wanapofika hospitali.

Mfumo huu wa dharura wa M-mama ulioagizwa utekelezwaji wake na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan unafanya kazi katika Mikoa 16 ya Tanzania bara Shinyanga, Mtwara, Lindi, Morogoro, Arusha, Manyara, Singida, Dodoma, Simiyu, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza, Mara, Mbeya, Songwe na Rukwa na Mikoa yote mitano ya Zanzibar.

# Tanzania ni Salama, Kagera ni Salama, Hakuna Ugonjwa wa Maburg.

Na Englibert Kayombo
WAF - Kagera.

Waziri wa Afya Mhe. ummy Mwalimu ameutarifu umma wa Watanzania na Ulimwengu kwa ujumla kuwa Tanzania imeweza kupambana na kudhibiti ugonjwa wa Marburg na hivi sasa kuwa Mkoa huo na nchi kwa ujumla ni salama na hakuna maambukizi ya ugonjwa huo.

Waziri Ummy alisema hayo kwenye kwenye kilele cha mapambano dhidi ya ugonjwa wa Marburg ambao uliripotiwa kuingia nchini mnamo Machi 16, 2023, Kagera Tanzania.

“Mwenyezi Mungu ametuwezesha, zimetimia zaidi ya siku 42 toka mgonjwa wa mwisho kupona Marburg, Kwa maana hiyo tumekidhi vigezo vya Shirika la Afya Duniani vya kutangaza mwisho wa ugonjwa wa Marbung, hivyo natangaza kwamba 02/06/2023 mlipuko wa ugonjwa wa Marburg tumeumaliza rasmi Mkoa wa Kagera” amesema Waziri Ummy Mwalimu.

Waziri Ummy alisema kuwa jitihada za pamoja za Serikali kwa kushirikiana karibu na Wadau wa maendeleo wa Sekta ya Afya na wa Kimataifa zimefanikisha mapambano hayo na kuweza kutangaza kutokomeza ugonjwa wa Marburg nchini ndani ya kipindi kifupi.

“Ni Fahari kwetu sisi Tanzania kwamba tumeweza kulinda Watanzania, tumeweza kutimiza wajibu wetu wa kimataifa wa kuilinda Dunia dhidi ya ugonjwa wa Marburg, nalishukuru sana Shirika la Afya Duniani kwa hapa Tanzania kwa kuongoza wadau wa kimataifa katika mapambano hayo” alishukuru Waziri Ummy.

Alisema kuwa mafanikio hayo ya kudhibiti ugonjwa wa Marburg ni juhudi za pamoja za Serikali kuanzia ngazi ya Taifa hadi jamii kwa kushirikiana na wadau wote.

“Ninawashukuru wataalamu wote wa afya Pia, natoa pongezi kwa viongozi wa kisekta na Watumishi wa sekta ya Afya kutoka Wizara ya Afya, OR-TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Taasisi za elimu nchini, Wananchi, wanahabari, sekta binafsi na wadau mbalimbali walioshirikiana nasi kwa hali na mali katika kukabiliana na ugonjwa huu” alisema

"Niendelee kuwaomba Wananchi nkuwa macho wakati wote na endapo kutatokea tetesi za mhisiwa au mtu mwenye dalili za ugonjwa wowote usio wa kawaida au unaotia mashaka ni vyema kutoa taarifa sehemu husika" alihimiza Waziri Ummy.





Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu akitoa tamko la kilele cha mapambano dhidi ya Ugonjwa wa Margurg Kagera, Juni 2, 2023



Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu akitoa taarifa ya kitaalam ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa Marburg nchini Tanzania, Juni 2, 2023, Kagera Tanzania.



Daktari Mahona Ndulu aliyeugua ugonjwa wa Marburg na kupona akiishukuru Serikali kwa kumsaidia na matibabu ya ugonjwa huo, Juni 2, 2023, Bukoba, Kagera Tanzania.



# Rais Samia anazidi kuifungua nchi, zaidi ya mataifa 120 wakutana Arusha kujadili masuala ya Afya

Na Rayson Mwaisemba, Arusha.

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amesema matokeo ya Filamu ya "Royal tour" iliyoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan yameendelea kuonekana baada ya nchi ya Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wataalamu wa masuala ya Afya zaidi ya 1200 kutoka nchi zaidi ya 106 unaoendelea Jijini Arusha.

Dkt. Mollel wakati akiongea na Waandishi wa habari baada ya ufunguzi wa Mkutano huo uliofunguliwa na Bishop Kisili Laizer kutoka Dayosis ya kati Tabora aliyemwakilisha Dkt. Fredrick Shoo katika Mkutano uliofanyika kwenye ukumbi wa kimataifa wa EACC Jijini Arusha.

Alisema, Mkutano huo ni mara ya pili kufanyika nchini Afrika ambapo mwaka huu Tanzania ndio mwenyeji wa Mkutano huo, hii ikiwa ni uthibitisho wa usalama, amani na uzuri wa nchi ya Tanzania ambao umekuwa ukitangazwa na Serikali.

Aidha, Dkt. Mollel alisema, ujio wa ugeni huu mkubwa una maana kubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi ya Tanzania kuanzia malipo ya ukumbi ambao ni zaidi ya Bilioni 1, huku akiweka wazi kwa mgeni mmoja anatumia zaidi ya 672,000 kwaajili ya malazi na vyakula na wengine wanaendelea kutembelea vivutio vyetu ikiwemi mlima Kilimanjaro, Ngorongoro pamoja na Serengeti.

Sambamba na hilo, Dkt. Mollel alisema, ujio huu una maana kubwa katika jitihada za Serikali kuelekea kwenye Health tourism, ambapo Wataalamu mbalimbali wa masuala ya Afya kutoka nchi mbalimbali wamekutana na kubadilishana uzoefu juu ya namna gani wataboresha huduma kupitia neno la Mungu.

Alisema, Rufaa za nje ya nchi zimepungua kwa 97% hii ni kutokana na uboreshaji katika mfumo wa afya ambapo kwa muda mfupi Serikali imetoa zaidi ya Trilioni 3 katika eneo la afya, huku mwaka jana ikiwa Trilioni 1 ambazo zimetumika katika kuboresha huduma na kununua vifaa tiba kwaajili ya matibabu.

Kwa upande mwingine aliwashukuru Waratibu wa wote wa Mkutano huo, kwa kuwakutanisha watu wa mataifa mbalimbali katika Mkutano huo, ambapo ni ishara ya kuisemea nchi ya Tanzania vizuri kwa mataifa hayo ndio sababu ya kukubali kwao kuja kufanya Mkutano huo katika nchi ya Tanzania.



# Serikali yakabidhi magari kwa ajili ya shughuli za usafi wa mazingira



Na Hassan Kimweri, Dodoma

Serikali kupitia Wizara ya Afya imekabidhi magari Sita yenye thamani ya Shilingi milioni 500 kwaajili ya kusaidia shughuli za maji na usafi wa mazingira katika Mikoa ya Shinyanga, Lindi, Simiyu, Katavi, Singida na Ruvuma.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Seif Shekalaghe Juni 9, 2023 amekabidhi magari hayo katika ofisi za Wizara ya Afya Jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga aliyewawalikisha Makatibu tawala wengine pamoja na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Dkt. Kheri Kagya.

Katika makabidhiano hayo Dkt. Shekalaghe amesema hii ni awamu ya pili ya utoaji wa magari hayo ambapo awamu ya kwanza yalitolewa Sita, huku akisisitiza kuwa Serikali itaendelea kutoa magari zaidi kwaajili ya uratibu wa shughuli za maji na usafi wa mazingira utakaosaidia kukabiliana na magonjwa mbalimbali kwa wananchi.





# Walimu, Wazazi na Jamii wahimizwa kuwahamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi

Na Mwandishi wetu
Dar Es Salaam.

Serikali imeendelea kuwaasa wazazi, walezi na jamii kuendelea kuhamasisha wanafunzi katika ngazi mbalimbali nchini kutambua umuhimu wa kusoma na kupenda masomo ya sayansi ili kuwatengeneza vijana kuwa wataalam wa kesho na kufikia malengo ya Mipango na Mikakati mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025).

Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Tumaini Nagu,alisesema hayo, Juni 1, 2023, katika hafla ya kuwapongeza wanafunzi waliofanya vizuri zaidi katika masomo ya sayansi (Biolojia, Fizikia na Kemia), kwa kidato cha nne na sita kwa mwaka 2021 na 2022, iliyofanyika katika Ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

"Sayansi inakua, na sisi kama wataalam ni lazima tuendelee kukua na kurithishana ujuzi na ufahamu unaoendelea kuboreshwa siku hadi siku. Ni lazima pia tufanye juhudi ya kuifanya jamii ione umuhimu wa sayansi na kutambua mchango kwa ustawi wa jamii na maendeleo ya taifa kwa ujumla" alisema Profesa Nagu.

Aidha, Mganga Mkuu wa Serikali, alisema kuwa moja kati ya vipaumbele vya Wizara ya Afya ni Kulinda afya ya jamii na mazingira, ambapo amesema utekelezaji wa kipaumbele hiki utaweza kufanikiwa kwa kujenga misingi ya kuandaa vijana wanaomudu na kupenda masomo ya sayansi, sambamba na kuimarisha vyuo vya mafunzo kwa wataalam wa sekta ya afya ya jamii.

"Ninashukuru kwamba Mamlaka imebuni mbinu bora na mwafaka ya kuhamasisha vijana kupenda masomo ya sayansi. Ni imani yangu kuwa, kazi hii ya kuwatia moyo vijana wetu waliofanya vizuri zaidi kwenye masomo ya sayansi itakuwa endelevu," alisema.

Sambamba na hilo, Profesa



Nagu, aliwapongeza Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mkemia Mkuu wa Serikali na watumishi wote wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), kwa kazi nzuri, kubwa na ngumu ambayo wamekuwa wakiifanya kwa moyo wa dhati, uzalendo na uadilifu na kuwasihi kuendelea na juhudi na moyo huo huo ili kuhakikisha Mamlaka inaendelea kutoa huduma bora kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake mwanafunzi aliyefanya vizuri zaidi katika somo la Kemia Kidato cha Sita, Lucy Elias Magashi, alipongeza utoaji wa zawadi hizo na kutoa rai kwa Serikali kuendelea kuhamasisha wanafunzi waliopo mashuleni kuendelea kusoma kwa bidii masomo mbalimbali hasa ya sayansi pamoja na kuwawezesha ili waweze kutimiza ndoto zao.

# “Tunaendelea kuboresha huduma za Sikoseli nchini” Dkt. Shekalaghe



Na Said Nyaoza, Dodoma.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Seif Shekalaghe amewahakikisha wadau wa Sekta ya Afya kuwa Serikali itaendelea kuboresha huduma za matibabu ya Sikoseli nchini.

Amesema hayo alipokutana na timu ya wawakilishi kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS) wanaosimamia mradi wa Sikoseli nchini wakiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo hicho Prof. Appolinary Kamuhabwa.

Katika kikao hicho kilichofanyika kwenye ofisi za Wizara Jijini Dodoma Katibu Mkuu Dkt. Shekalaghe ameihakikishia timu hiyo juu ya kuendelea kuboresha Sekta ya Afya hususan katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa Sikoseli nchini.

“Juhudi zinaendelea kufanywa na Serikali na wadau mbalimbali katika huduma za kuzuia na kudhibiti ugonjwa wa Sikoseli zikiwemo tafiti za kisayansi, upatikanaji wa matibabu ya hali ya juu kwa wagonjwa wa Sikoseli kama ubadilishaji damu na upandikizaji uloto.” Amesema Dkt. Shekalaghe

Aidha, wamejadiliana ukubwa wa ugonjwa wa Sikoseli nchini ambapo Mkurugenzi wa Jumuia hiyo Bi. Arafa amesema kuwa, watoto 11,000 hadi 14,000 huzaliwa na ugonjwa wa Sikoseli kila mwaka na inakadiriwa kuna jumla ya wagonjwa ni 200,000 wa Sikoseli nchini Tanzania.

Vile vile, timu hiyo imesema kuwa takribani asilimia 12 hadi 20 ya Watanzania wana vinasaba vya Sikoseli ambao wanaweza kupata watoto wenye ugonjwa wa s
Sikoseli na kuongeza idadi ya wagonjwa wenye ugonjwa huo hapa nchini.

Timu hiyo iliyoongozwa na Prof. kamuhabwa ameambatana na Makamu Mkuu wa Chuo Elimu na Matafiti Mkuu wa Mradi wa Sikoseli Prof. Emmanuel Balandya, Mkurugenzi wa Jumuiya ya wagonjwa wa Sikoseli Tanzania Bi. Arafa Saidi, Watafiti katika mradi wa Sikoseli Dkt. Irene Minja, Dkt. Siana Nkya na Lulu Chirande








# Waziri Ummy Mwalimu azindua Baraza jipya la Madktari Tanganyika.

Na Englibert Kayombo
Dodoma.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amezindua Baraza jipya la Madaktari Tanganyika linalotarajia kudumu kwa muda wa miaka mitatu, huku moja ya jukumu la Baraza hilo ni kumshauri Waziri wa Afya katika masuala ya udhibiti, utoaji huduma na mafunzo kwa wataalamu wa Udaktari, Udaktari wa Meno na Afya Shirikishi.

Waziri Ummy amezindua Baraza hilo leo Juni 7, 2023 katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma, tukio lililohudhuriwa na Wakurugenzi wa Wizara, Wasajili wa Mabaraza, Wasajili wa bodi na Watumishi mbalimbali wa Wizara ya Afya.

Katika tukio hilo, Waziri Ummy ameelekeza Baraza kusimamia viapo na maadili ya taaluma zao yanavyoelekeza, hususan kwenye suala la kuokoa maisha ya mgonjwa kwanza kabla ya kutanguliza maslahi binafsi ikiwemo ya fedha jambo ambalo ni kinyume na viapo na maadili ya taaluma ya Udaktari.

Ameendelea kusema, taaluma ya Udaktari lazima kuwe na ubora elekezi (standards) kwakuwa inahusu maisha ya watu na amepongeza Baraza hilo lililomaliza muda wake kwa kazi nzuri waliofanya katika hili.

Aidha, Waziri Ummy amesema Pamoja na kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na Baraza lililomaliza muda wake, bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika kusimamia Madaktari, huku akitaka kujua katika miaka mitatu ya Baraza ni madaktari wa ngapi wamechukuliwa hatua za kusimamishiwa sajili zao au kupewa onyo katika kipindi hicho.

Sambamba na amelitaka Baraza jipya kukaa na TCU ili kuona mahitaji ya soko la ajira katika kada za Udaktari ili kuwasaidia wanafunzi wasome kulingana na mahitaji ya soko la nchi katika fani ya Udaktari hali itayosaidia kupunguza idadi ya Wataalamu wasio ajirika nchini. Kwa upande wake, Mwenyekiti-wa Baraza la Madaktari Tanganyika Prof. David Ngasapa amesema Baraza lina mamlaka ya Kimahakama (Quasi - Judicial) inayolipa uwezo wa kuendesha uchunguzi na kumshitaki Mwanataaluma yeyote ambaye atatuhumiwa kwenda kinyume na maadili ya taaluma ambayo imewekwa na Sheria pamoja Kanuni za Maadili ya Kitaaluma.

Sambamba na hilo, Dkt. Mollel amesema, Serikali ya Rais Samia imeweka fedha nyingi katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza, ikiwemo eneo la manunuzi ya vifaa tiba ikiwemo CT-SCAN katika kila hospitali ya Rufaa ya Mkoa pamoja kusaini mikakati kwa Wakuu wa Mikoa wote kuhusu masuala ya lishe kwenye kila mkoa.

Kwa upande mwingine, Dkt. Mollel amesema Mkakati mwingine wa mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza ni kuunga mkono kwa Mpango wa Bima ya Afya kwa wote pindi utapoletwa Bungeni ili kumpa haki kila mwananchi kupata matibabu bila malipo kuanzia ngazi ya Zahanati hadi hospitali ya Taifa.

# Wazalishaji wadogo wa chumvi watakiwa kuzalisha chumvi zenye madini joto.



Na Emmanuel Malegi,
Dar Es Salaam.

Naibu katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe ameitaka kamati ya Taifa ya Kudhibiti Upungufu wa Madini joto nchini, kuhakikisha inasimamia na kufuatilia wazalishaji chumvi wadogo nchini kuhakikisha chumvi wanayozalisha nchini inawekewa madini joto ili kuweza kupunguza athari za kiafya zinazoweza kujitokeza kwa watumiaji wa chumvi watakaokosa madini hayo muhimu mwilini.

Dkt. Magembe amebainisha hayo wakati wa uzinduzi wa Mkutano wa 55 wa Kamati ya Taifa ya Kudhibiti Upungufu wa Madini Joto nchini, ambao umefanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania jiji Dar es Salaam.

Naibu Katibu Mkuu Dkt. Maghembe amesema hawana shaka na chumvi inayozalishwa na viwanda vilivyopo nchini juu ya uongezaji wa madini joto, ila kuna wazalishaji wadogo wapo ambao hawaongezi madini joto kwenye chumvi wanayozalisha, na chumvi hiyo imekuwa ikiingizwa sokoni katika maeneo yao na kutumiwa na wananchi.

“Suala la kuvuna chumvi linalofanywa na wazalishaji wadogo ni ajira na hauwezi kuwakataza wasivune chumvi ambayo inawaingizia kipato,ila ni lazima tuchakate vichwa vyetu na kuhakikisha wazalishaji wadogo hawa wanazingatia sheria na taratibu zilizowekwa kwa kuhakikisha chumvi wanayozalisha inawekewa madini joto.

Aidha Dkt. Magembe ameitaka kamati hiyo kuhakikisha elimu ya umuhimu wa madini joto inatolewa kwa wazalishaji chumvi wadogo, na kuwaelimisha umuhimu wa kutumia chumvi iliyoongezwa madini joto na athari za kiafya anazoweza kuzipata mtu ambaye hatotumia chumvi ambayo imeongezwa madini joto.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania Dkt. Germana Leyna amesema lishe ni suala mtambuka na limekuwa likiwakutanisha wadau wengi pamoja, na kila mdau amekuwa na majukumu yake katika kuhakikisha lishe ya Mtanzania imekaa vizuri.

Dkt. Leyna amesema kamati hiyo ya kitaifa imekuwa ikijipambanua kufuatilia na kuhakikisha chumvi inayozalishwa nchini inaongezwa madini joto ya kutosha ili kuwaepusha watanzania na athari za kiafya wanazoweza kuzipata kwa kukosa madini hayo muhimu mwilini.

Akiwasilisha taarifa ya juu ya programu ya kuzuia Upungufu wa madini joto nchini, mratibu wa programu hiyo Bi. Rose Msaki amesmea matumizi ya chumvi yenye madini joto kwa hapa nchini yameongeza ila bado hatujaweza kufikia kiwango kilichoweka na Shirika la Afya Duniani (WHO) hivyo kupitia kamati hiyo kila mjumbe ameweza kupewa jukumu la kuhakikisha anashiriki kikamilifu kusimamia chumvi inayozalishwa nchini inaongezewa madini joto.



# Karibu Tanzania Dkt. Charles Sagoe-Moses, Kwaheri Dkt. Zabron Yoti

Na Catherine Sungura, Dodoma.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu tarehe 08 Juni 2023 alimkaribisha Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) nchini Tanzania Dkt. Charles Sagoe-Moses.

Waziri Ummy amempongeza na kumkaribisha Dkt. Sagoe-Moses na amemuahidi kumpa ushirikiano ili kwa pamoja waweze kuboresha sekta ya afya nchini.

Kwa upande wake Dkt. Sagoe-Moses ameahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya ili Watanzania waweze kupata huduma bora za afya.



Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu (kushoto) akimkabidhi zawadi Mwakilishi Mkazi aliyemaliza muda wake nchini Dkt. Zabron Yoti, Juni 8, 2023.



Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu (kushoto) akimkabidhi zawadi Mwakilishi Mkazi wa Shirikal la Afya Duniani Dkt. Zabron Yoti aliyemaliza muda wake nchini Tanzania, Juni 8, 2023.

# Dhamira ya Serikali ni kuimarisha huduma za afya kwa wananchi.

Na Rayson Mwaisemba, Dodoma..

Mfamasia Mkuu wa Serikali Bw. Daudi Msasi amesema kuwa mwelekeo wa Wizara ya ni kuhakikisha huduma za afya zinazotolewa katika vituo vyote nchini hasa huduma za dawa zinaboreshwa ili wananchi wa hali zote wanufaike na huduma hizo.

Bw. Msasi amebainisha hayo leo Juni 10, 2023 alipotembelea katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma (General) katika Famasi ili kujionea hali ya upatikanaji wa dawa ikiwa ni kuelekea maadhimisho ya wiki ya Famasi yenye kilele chake Juni 16 Jijini Dodoma, huku kauli mbiu ikiwa "Famasi ni nguzo ya mfumo wa huduma za afya ulio madhubuti, thabiti na bora".

"Mwelekeo wa Wizara ya Afya ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha ubora wa huduma za afya kwa wananchi na ndio lengo kubwa." Amesema Bw. Daudi Msasi.

Amesema, upatikanaji wa dawa ni nguzo muhimu katika suala la ubora wa huduma, hivyo ameishukuru Serikali ya Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za kutosha kwenye eneo la dawa, miundombinu, vifaa na vifaa katika vituo vyote nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora katika vituo vyote.

Aidha, Bw. Msasi amewashukuru Wafamasia wote nchini kwa kuendelea kujitoa katika kutimiza majukumu yao ikiwemo katika kusimamia upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma na eneo la elimu kwa wananchi ili kuongeza matumizi sahihi ya dawa na kuondoa changamoto ya usugu wa vimelea vya maginjwa dhidi ya dawa.

Nae, Kaimu Mkuu wa Idara ya Famasi ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha huduma tabibu za kifamasia katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma Bw. Soud Nasoro Soud ametoa wito kwa Wafamasia wote nchini kuzingatia miiko na maadili ya viapo vya taaluma ya Wafamasia ili kuhakikisha hakuna changamoto inayompata mgonjwa kwenye suala la upatikanaji wa huduma ya dawa katika vituo vya kutolea huduma.

Kwa upande wake Bw. Athanas Macheyeki ambae ameenda kupata huduma ya dawa katika famasi iliyopo katika hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Dodoma ameishukuru Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kuendelea kuboresha huduma hasa katika upatikanaji wa dawa ili wananchi waweze kusaidika kupata huduma kwa urahisi.

"Kwakeli naipongeza sana Serikali chini ya mama yetu Rais. Dkt. Samia Suluhu Hasaan kwa kuwajali wananchi wake kwa upatikanaji wa huduma kwa haraka hasa katika eneo la upatikani wa dawa akisaidiwa na wasaidizi wake akiwemo Waziri Mhe. Ummy Mwalimu ambaye ni Waziri wa afya." alisema Bw. Macheyeki.




Bw. Daudi Msasi, Mfamasia Mkuu wa Serikali


# Mazoezi kwa afya bora



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe Juni 11, 2023 aliongoza wananchi kwenye Marathon ya Jiji la Dodoma maarufu kwa jina la Capital City Marathon zilizofanyika Chimwaga Dodoma.

Dkt. Magembe amewakumbusha wananchi kujenga mazoea ya kufanya mazoezi ya mara kwa mara ili kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza.







# Serikali kuendelea kushirikiana na Wadau wa Sekta ya Afya katika mapambano dhidi ya VVU

Na Hassan Kimweri, Dodoma.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu, Juni 12, 2023 alikutana na Mratibu wa Jitihada za Kimataifa za Marekani za kukabiliana na UKIMWI, Balozi John Nkengasong kwa pamoja wametembelea Kikundi cha Chamwino Kuona utolewaji wa huduma jumuishi na uwezeshaji kiuchumi.

Katika kikao hicho kifupi kilichofanyika katika shule ya msingi Chamwino Jijini Dodoma Waziri Ummy aliwataka Mabinti hao kwa wenye utayari wa kurudi shule warudi, kwakuwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa ruhusa ya kurudi shule watoto wote waliokatisha masomo yao kutokana na kupata ujauzito wakiwa shuleni.

"Naona mabinti wengi ni wadogo wengine mmekatisha masomo yenu kutokana na kupata mimba hivyo tumie fursa hii ya kurudi shule ili muendelee na masomo yenu na mtimize ndoto zenu". Alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alimtaka Mganga Mkuu wa Mkoa (RMO) Dkt. Best Magoma awaunganishe watoto hao wanaotaka kurudi shule na Afisa Elimu Mkoa ili wanaotaka kurudi Sekondari warudi kwakutumia vizuri fursa iliyotolewa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Lengo la kuwatembelea hapa ni kuangalia utekelezaji wa afua za kuzuia maambukizo ya VVU kwa wasichana balehe na wanawake vijana wa umri wa miaka 15 hadi 24 na Kuona utolewaji wa huduma jumuishi na uwezeshaji kiuchumi". Alisema Waziri Ummy

Kwa upande wake Balozi Nkengasong aliwapongeza mabinti hao kwa kutumia dawa kinga kwaajili ya kuzuia maambukizi zaidi ya UKIMWI na kuwataka kuyafanyia kazi yale yote waliyofundishwa ili kufikia malengo yao.

"Lakini pia tumepokea maombi yenu kwa pamoja tutayajadili kwa kuona namna gani tunayafanyia kazi haraka iwezekanavyo ikiwemo la kuwasaidia namna gani mtajikwamua hapa mlipo na kuendeleza biashara zenu". Alisema Balozi Nkengasong

Nae, Victori Samweli Binti mwenye umri wa miaka 11 aliomba awezeshwe kwa kusaidiwa mtaji au kurudi shule ili atimize ndoto zake za kusaidia familia yake na jamii kwa ujumla.

"Ndoto yangu kubwa ni kuwa mjasiliamali mkubwa ili niweze kusaidia mabinti waliyopo katika mazingira hatarishi pia waweze kuachana na tabia hatarishi kama kujiingiza katika mahusiano ya kingono katika umri mdogo." Alisema Binti Victori

> "Naona mabinti wengi ni wadogo wengine mmekatisha masomo yenu kutokana na kupata mimba hivyo tumie fursa hii ya kurudi shule ili muendelee na masomo yenu na mtimize ndoto zenu". Amesema Waziri Ummy




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na Mratibu wa Kimataifa wa Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani katika mwitikio wa kupambana na Ukimwi (PEPFAR) na Mwakilishi Maalum wa Serikali ya Marekani katika masuala ya Diplomasia ya Afya Balozi Dkt. John Nkengasong, Mwakilishi Maalum wa Global Health Diplomacy na Makamu Mkurugenzi Mtendaji wa masuala ya Program wa UNAIDS, Bi Angeli Achrekar, Mtendaji Mkuu wa Shirika la Kimataifa la kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund) Bw. Peter Sands, Katibu Mkuu Kiongozi Dkt. Moses Kusiluka na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu, mara baada ya mazungumzo yao Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma tarehe 12 Juni 2023.





# Kwenye kila watu 100 wanaokadiriwa kuwa na VVU, 86 wanajua hali zao za kiafya.

Na Said Nyaoza,
Dodoma



Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amebainisha kuwa katika kila watu 100 wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya Virusi vya Ukimwk watu 86 wanajitambua hali zao ambapo kati yao 97% wanatumia dawa.

Waziri Ummy aliyasema hayo Juni 12, 2023 wakati alipotembelea katika Kituo cha Afya MAKOLE akiambatana na Waziri wa TAMISEMA Mhe. Angera Kairuki pamoja na ugeni kutoka mfuko wa Rais wa Marekani wa kupambana na Ukimwi US-PEPFAR, Global Fund na UNAIDS Jijini Dodoma.

“Tunawashukuru wadau wetu hawa kwa msaada mkubwa waliotupatia ambao umeisadia Tanzania kupatikana kwa mafanikio makubwa ambayo yameweza kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) ambapo katika kila watu 100 wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU, watu 86 wanajitambua kuwa wanamaambukizi baada ya kupima na kati yao 97% wanatumia dawa”. Alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alisema kuwa katika kila watu 100 Tanzania wenye maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na wanaojua hali zao ni asilimia 97 ambao wanatumia dawa na wamefanikiwa kufubaza virusi hivyo kwa kujiepusha na maambukizi ya magonjwa mengine na wanaweza wasiwaambukize watu wengine.

Alisema kuwa lengo la Ugeni huo nchini Tanzania umekuja kuangalia utendaji na utekelezaji wa afua mbalimbali za kupambana na Ukimwi, TB na Maleria na kuona uwezekano wa kuongeza nguvu ili kupunguza maambukizi ya magonjwa hayo.

Pia, Waziri Ummy alisema tatizo hili limewakumba sana wanaume hivyo Serikali itaendelea kuchukua mikakati mbalimbali ya kuwashawishi wanaume kupima UKIMWI ili kuweza kutambua hali ya maambukizi ya VVU.

“Lakini pia kundi lingine linalopata maambukizi kwa wingi ni wasichana balehe ambao wanafanya kazi kwenye mabaa, mahoteli, makasino na kwenye vijiwe kwahiyo hao nao tutaweka mikakati mbalimbali ya kuwafikia”. Alisema Waziri Ummy.

Waziri Ummy alisema eneo la tatu watakalokwenda kulifanyia kazi ni maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ambapo Dunia inataka iwe asilimia 5 lakini kwa Tanzania ni asilimia 6.5 ya watoto wanaozaliwa na maambukizi.

Mwisho, Waziri Ummy alitoa wito kwa Watanzania hasa wanaume kwenda kupima kujua hali zao lakini kwa ambao wanajua hali zao dawa za UKIMWI zipo na zinatolewa bila malipo na vipimo vya kujipima mwenyewe vipo kwahiyo Watanzania wajitokeze kupima ili tutokomeze UKIMWI ifikapo mwaka 2030.



# Zaidi ya Wanafunzi 342,933 Wasajiliwa na NHIF

Na Rayson Mwaisemba

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amebainisha kuwa Serikali kupitia mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya mpaka kufikia Machi 2023 umeshasajili jumla ya wanafunzi 342,933 ikiwemo wa Shule za msingi, Sekondari na Vyuo vya Kati unaotoa nafasi kwa wananchi hao kupata matibabu bila malipo katika vituo vyote vinavyotoa huduma za NHIF.

Dkt. Mollel alisema hayo Juni 15, 2023 wakati akijibu swali la Mbunge wa viti maalumu Mhe. Lucy John Sabu, Bungeni Jijini Dodoma.

“Hadi kufikia Machi 2023, Mfuko umeshasajili jumla ya wanafunzi 342,933 ikiwemo wa Shule za msingi, Sekondari na Vyuo vya Kati.”

Aliendelea kusema, zoezi hili la kusajili wanafunzi ni endelevu kupitia shule na vyuo ili kuhakikisha wanafunzi wengi zaidi kuingia katika mfuko huo ili wapate huduma bila malipo, huku akisisitiza kuwa, wanafunzi watatakiwa kuchangia shilingi 50,400 ili kupata bima ya matibabu.





# Tutaendelea kudumisha uhusiano wetu na Namibia

Na Catherine Sungura
Dodoma.

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya na Serikali ya Namibia itaendelea kushirikiana kwa pamoja hasa katika sekta ya afya kwa kuwa nchi hizo mbili zimekuwa na historia nzuri ya kuimarisha mifumo ya afya.

Alisema hayo Juni 13, 2023 na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu wakati wa kikao na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Usawa wa Kijinsia, Maendeleo ya Jamii na Mambo ya Familia kutoka nchini Namibia kilichofanyika katika hospitali ya Benjamin Mkapa Jijini Dodoma.

"Kwa kutambua urafiki wa nchi zote mbili, naamini urafiki wetu umekuwa na manufaa sana katika mfumo wa huduma za Afya wa Tanzania lakini pia tunakushukuru kwa kutembelea nchi yetu na ninaamini tutaendelea kuwa na uhusiano mzuri kwa kuwahudumia wananchi wetu." Alisema Waziri Ummy

Aidha, katika kikao hicho Waziri Ummy na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Usawa wa Kijinsia, Maendeleo ya Jamii na Mambo ya Familia kutoka nchini Namibia walijadiliana mambo mbalimbali yanayohusu afya ikiwemo masuala ya Ubora wa afya ya Umma, Utekelezaji wa mpango mkakati wa hali ya afya katika kupambana na magonjwa yakiwemo magonjwa yasiyoambukiza.

Pia, walijadiliana hali ya upatikanaji wa huduma za afya na miundombinu, gharama ya huduma ya afya ya Umma kwa lengo la kujifunza na kuona huduma hizo zinavyotolewa Nchini Tanzania.
Katika upande wa upatikanaji wa huduma za afya na miundombinu Waziri Ummy alisema Huduma ya afya nchini Tanzania inatolewa kupitia mchanganyiko wa sekta za umma na binafsi ambapo Wizara ya Afya ina jukumu la kusimamia na kuratibu huduma za afya nchini.

"Hivi sasa hapa nchini tuna jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 11,040 ambavyo vinajumuisha vituo vya umma 6,682 na kwa utendaji kazi wake tuna Hospitali 430, vituo vya Afya 1,030, zahanati 1,458 na maabara za binafsi 1,206". Alisema Waziri Ummy

Mwisho, Waziri Ummy alisema huduma za Afya ya Msingi imeimarishwa kwa kujenga miundombinu kwa kutumia ufadhili wa UVIKO-19 ikiwemo Idara za wagonjwa wa nje na za Dharura.

# Waziri Ummy aagiza vituo vyote vya upasuaji kuwa na majokofu ya kuhifadhi mazao ya damu



Na Emmanuel Malegi, Dodoma.

WAZIRI wa Afya , Mhe. Ummy Mwalimu, ameviagiza vituo vyote vya afya nchini vinavyotoa huduma za upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni kuwa na majokofu ya kuhifadhia mazao ya damu (Plasma) ili kusaidia kupunguza vifo vya wajawazito vitokanavyo na kutokwa damu nyingi wakati wa kujifungua.

Waziri Ummy, alisema hayo leo jijini Dodoma, kwenye maadhimisho ya siku ya Mchangiaji damu Duniani pamoja na uzinduzi wa Kituo cha Damu salama Kanda ya kati.

Waziri Ummy alisema ili kuondokana na vifo vya wajawazito wakati wa kujifungua vituo vyote vya afya nchini vinapaswa kuwa na majokofu ya kuhifadhia mazao ya damu.

“Akinamama wengi wamekuwa wakipoteza maisha yao wakati wa kujifungua kutokana na kutokwa damu nyingi pamoja na uwepo wa sindano zinatumika kuzuia kutoka kwa damu lakini uwepo wa damu katika kituo ni jambo la lazima sana ili kuokoa maisha ya mama”alieleza Waziri Ummy

Pia alisema sababu nyingine ya vituo hivyo kuwa na majokofu ya kuhifadhina mazao ya damu ni kutokana na damu kuwa na uwezo wa kutumia ndani ya siku 45 pekee na baada ya muda huo inaharibika.


“Damu baada ya mtu kuchangia na kuhifadhiwa kwenye kituo cha damu salama inaweza kutumika ndani ya siku 45 na baada ya hapo inaharibika hivyo kutokana na teknolojia kukua inaweza kutengenezwa mazao ya damu (plasma) na kuwa na uwezo wa kudumu kwa mwaka mmoja”alisema




Aidha, aliagiza halmashauri zote nchini kutenga bajeti kwa ajili ya kuhamasisha na kukusanya damu katika maeneo yao ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

Vile vile alisema jukumu la kukusanya damu ni la kila halmashauri hivyo wahakikishe wanatenga bajeti ambayo itawawezesha kukusanya damu na kuihifadhi katika benki zao kwa ajili ya matumizi.

“Leo hii halmashauri ukisikia kuna mechi ya Simba na Yanga peleka timu watu wachangie damu, ukisikia kuna tukio la serikali peleka timu pia watu wachangie na hili liwe ni kipaumbele katika majukumu yenu ya kila siku kwani damu ni jambo la muhimu sana hakuna duka wala kiwanda kinacho uza damu ni sisi wenyewe ndiyo tutachangiana”aliongeza Waziri Ummy.



# Shilingi Bilioni 5 zimetengwa kugharamia huduma za upasuaji na matibabu ya kibingwa

Na Hassan Kimweri, Dodoma.

Serikali kupitia Wizara ya Afya imetenga kiasi cha shilingi Bilioni 5 kwaajili ya kugharamia huduma za upasuaji na matibabu ya ubingwa bobezi ili kurahisha upatikanaji wa huduma hizo kwa Watanzania wenye hali zote.

Waziri Ummy alisema hayo leo kwenye ufunguzi wa Kongamano la 28 na Mkutano Mkuu wa Chama cha Madaktari wa Upasuaji nchini Tanzania unaofanyika kwa siku tatu Jijini Dodoma.



"Huduma hizo za upasuaji na matibabu ya ubingwa bobezi zitapatikana hapa hapa kwetu Tanzania, kwa mfano hospitali ya Benjamini Mkapa walivyofanya katika upandikizaji wa ULOTO ambao umegharimu shilingi milioni 58, na Serikali imetenga Bilioni 5 ambapo tunaweza kupata wagonjwa 100". Alisema.

Aidha, Waziri Ummy alisema, Serikali inaanza mchakato wa kuwasambaza upya Madaktari Bingwa nchini ili kutatua changamoto ya uhaba wa madaktari hao katika maeneo yenye uhitaji mkubwa Mikoani.

"Lakini pia sisi kama Serikali tutajitahidi kuboresha maslahi yenu (Madaktari Bingwa wa Mifupa) na maslahi ya wafanyakazi wengine katika vituo va kutolea huduma za afya nchini". Ameongeza Waziri Ummy.

Pia, Waziri Ummy alizitaka hospital za Muhimbili, MOI, JKCI na Mloganzira kutoajiri Madaktari mojo kwa moja kutoka vyuoni bali wawachukue walio Mikoani ambao wamekuwa na uzoefu wa muda mrefu katika utoaji huduma.

"Nimeshapeleka mapendekezo haya kwa wenzetu wa utumishi kwamba (Muhimbili, MOI, JKCI na Mloganzira) wasiajiri Madaktari mojo kwa moja kutoka vyuoni bali wawachukue walio Mikoani ambao wamekuwa na uzoefu wa muda mrefu na hawa wapya ndio tuwapeleke Mikoani". Alisema Waziri Ummy

Alisema, Nchi yetu bado inauhitaji mkubwa wa Madaktari Bingwa na Ubingwa Bobezi ikiwemo Madaktari wa Upasuaji, hivyo Serikali itaendelea kutenga fedha ili kusomesha Wataalam wengi zaidi katika ngazi ya Ubingwa na Ubingwa bobezi.




Hata hivyo, Waziri Ummy alisema kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya inatambua uwepo wa changamoto ya fedha za matibabu kwa Watananzia ndio maana tumekuja na swala la Bima ya Afya kwa Wote (NHIF).

"Tunatambua matibabu yamekuwa na gharama hivyo Bima ya Afya kwa Wote ndio itawezesha Watanzania kupata huduma kwa urahisi ndio maana tupo tunaendelea na mchakato wa kupitishwa." Alisema Waziri Ummy.

Sambamba na hilo, Waziri Ummy alisema, Serikali iko tayari kuyapokea na kuyafanyia kazi maazimio yatakayotokana na kikao hiki ambayo naamini yatakuwa yenye malengo mahususi kwaajili ya uboreshaji katika Sekta ya afya.

Kauli mbiu ya Kongamano hilo la 28 na Mkutano Mkuu huo wa mwaka huu inasema "KUJENGA MFUMO WA UTOAJI HUDUMA ZA UPASUAJI MADHUBUTI, UNAOFIKIKA NA WENYE CHARAMA NAFUU TANZANIA"




Maandamano ya kuadhimisha Siku ya Sikoseli Duniani ambayo yameanzia katika viwanja wa Nyerere Square Jijini Dodoma kuelekea katika Kituo cha Afya Makole. Siku ya Sikoseli Duniani huadhimishwa kila tarehe 19 ya Mwezi wa Sita ambapo mwaka huu yamekuja na kaulimbiu isemayo "VUNJA MDUALA, PIMA JUA HALI YAKO YA SIKOSELI".

# Watoto 20 wenye Sikoseli kupandikizwa Uloto bila malipo

Na Majid Abudlkarim
Dodoma.

Serikali kupitia Wizara ya Afya itagharamia matibabu ya Watoto 20 wenye ugonjwa wa Sikoseli kwa kupandikizwa Uloto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Benjamini Mkapa (BMH) bila malipo.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu leo tarehe 19 June 2023, kwenye Maadhimisho ya Siku ya Sikoseli Duniani ambapo Kitaifa yamefanyika katika kituo cha afya Makole Jijini Dodoma.

Waziri Ummy alisema kuwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa kiasi cha Shilingi Bilioni 5 kugharamia huduma za ubingwa bobezi ikiwemo upandikizaji wa uloto kwa watoto wenye sikoseli 20, hivyo amewataka wataalam wa upandikizaji huo kujiandaa kwa ajili ya kutoa huduma hiyo.

"Mwaka huu naomba wazazi au walezi ambao mna watoto muwapeleke Hospitali kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na nimetoa changamoto kwa Benjamin Mkapa wapandikize watoto 20 ambao watadhaminiwa kwa asilimia 100 na Rais Samia Suluhu Hassan, hakutakuwa na kuchangia". Alieleza Waziri Ummy.

Aidha, Waziri Ummy alimpongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Wizara ya Afya zaidi ya Shilingi bilioni 5 kwa ajili ya huduma za ubingwa bobezi ikiwemo kupandikiza uloto kwa watoto 20.

Gharama za upandikizaji wa uloto kwa wagonjwa wa selimundu zinatajwa kuwa kati ya Shilingi milioni 55 kwa mgonjwa mmoja nchini wakati nje ya Nchi matibabu hayo ni Shilingi milioni 120 hadi 150.

Matibabu ya uloto uhusisha uvunaji, uchakataji, na upandikizaji wa chembe chembe hai mama za damu. Pia ametoa wito kwa wazazi kwenda kwenye kliniki za Sikoseli katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda na Vituo vya Afya, hivyo mtu anaweza kuanzia katika kituo cha afya kama Makole (Dodoma) watakao waunganisha na Hospitali ya Benjamini Mkapa na Hospitali ya Taifa Muhimbili Mei 10 mwaka huu Hospitali ya BMH ilianza kutoa huduma ya kupandikiza uloto ambapo watoto watatu waishio na ugonjwa wa Sikoseli walipandikiziwa huduma hiyo.

Hospitali ya Benjamin Mkapa ni ya pili nchini kutoa huduma hiyo muhimu baada ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), ambayo yenyewe ilianza kutoa huduma hiyo rasmi mwaka 2021.



# Serikali yatoa Shilingi Bilioni 3.6 kuboresha miundombinu JKCI

Na Mwandishi wetu, JKCI
Dar Es Salaam.



Shilingi Bilioni 3.6 zimetolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suhulu Hassan kujenga jengo la Utawala na vipimo ikiwa ni sehemu ya kuboresha huduma zinazotolewa na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI).

Jengo hilo linalotarajiwa kumalizika mwezi Agosti mwaka huu linatarajiwa kutoa huduma za vipimo kwa wagonjwa zaidi ya 200 kwa siku hivyo kupunguza muda wa kusubiri huduma za vipimo na matibabu ya moyo.

Akizungumza wakati wa ziara ya kuangalia maendeleo ya ujenzi wa jengo hilo Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Seif Shekalaghe alisema kutokana na ongezeko la mahitaji ya huduma za matibabu ya moyo Mhe. Rais alitoa fedha hizo ili kuhakikisha kuwa huduma za matibabu ya moyo zinaboreshwa hapa nchini.

“Jengo moja lililopo kwa sasa linahudumia wagonjwa wa nje, linatoa huduma za vipimo, kutoa huduma za upasuaji wa moyo pamoja na kulaza wagonjwa hivyo kuleta msongamano mkubwa kwa wagonjwa wanaopata huduma JKCI”, alisema Dkt. Shekalaghe.

Dkt. Shekalaghe alisema Wizara inafuatilia hela zinazotolewa na Mhe. Rais ili ziweze kukidhi mahitaji yaliyokusudiwa kwa wakati hivyo kuwataka wakandarasi wa ujenzi huo kufanya kazi usiku na mchana ili ujenzi uweze kukamilika kwani Mhe. Rais anapenda anapotoa fedha zitumike kama zilivyopangwa ili aweze kutoa tena fedha nyingine katika kuboresha sekta ya afya.

“Hadi sasa jengo hili limekamilika kwa asilimia 71, natambua kwamba ujenzi huu upo nyuma ndani ya mwezi mmoja kwani lilitakiwa kukamilika mwezi Mei mwaka huu, baada ya ziara ya leo naomba kusiwe na changamoto nyingene tena kuzuia jengo hilo kukamilika mwezi Agosti”, alisema Dkt. Shekalaghe.

Aidha Dkt. Shekalaghe alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI kuhakikisha kuwa vifaa vinavyohitajika katika jengo hilo vinaandaliwa mapema ili jengo linapokamilika mwezi wa nane lianze kutumika hapo hapo na kusiwe na changamoto za kusubiria vitendea kazi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Dkt. Peter Kisenge alisema kumekuwa na uhaba mkubwa wa ofisi pamoja na vyumba vinavyotoa



huduma za vipimo vya moyo hivyo Rais Samia alipotembelea Taasisi hiyo mwaka jana kwa ajili ya kuzindua mtambo wa Cathlab akawiwa kutoa fedha hizo lengo likiwa kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa na Taasisi hiyo.

Dkt. Kisenge alisema wagonjwa wa moyo wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu kupata huduma za vipimo vya moyo hivyo kumalizika kwa jengo hilo kutawapa nafuu wagonjwa kutokusubiri huduma za vipimo hasa upande wa kipimo cha kuangalia jinsi moyo unavyofanya kazi (Echocardiograph – ECHO).

"Mitambo itakayowekwa katika jengo la utawala na vipimo vya moyo itakuwa mikubwa na ambayo inachukua muda mfupi kutoa huduma za vipimo na majibu ambapo tunatarajia ndani ya masaa mawili mgonjwa anaweza kuwa ameshafanyiwa vipimo, kupatiwa majibu yake, na kumuona daktari", alisema Dkt. Kisenge.

Dkt. Kisenge alisema jengo la utawala na vipimo litatoa huduma za maabara, huduma za vipimo vya ECHO na ECG, eneo maalum kwa ajili ya wagonjwa wanaotoka nje ya nchi (Medical Tourism), lakini pia kama alivyoshauri Katibu Mkuu Wizara ya Afya kutakuwa na vyumba vya madaktari kwa ajili ya kuwaona wagojwa ili kuwapunguzia mzunguko wagonjwa.

Naye Mkandarasi wa jengo hilo kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Baraka Killungu alisema jengo hilo lenye ukubwa wa mita za mraba 1400 lina ghorofa 4 ambapo kila ghorofa lina ukubwa wa mita za mraba kati ya 290 hadi 330.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Seif Shekalaghe akisalimiana kwa furaha na Mtoto Sefu Msafiri Ablahi aliyelazwa katika wodi ya watoto wenye magonjwa ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) Jijini Dar Es Salaam. Dkt. Shekalaghe alitembelea Taasisi hiyo kuona hali ya utoaji huduma, uboreshaji wa miundombinu na kisha kuzungumza na Menejimenti ya Watumishi JKCI Juni 19, 2023.

# Wanafunzi 150 wa Udaktari kutoka Sudan wahamishiwa Muhimbili.



Na Mwandishi wetu,
Dar Es Salaam.

Wanafunzi 150 wa udaktari kutoka Chuo Kikuu cha Tiba, Sayansi na Teknolojia (UMST) cha Khartoum nchini Sudan wamehamishiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ili kukamilisha mwaka wao wa mwisho wa masomo.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kuwakaribisha wanafunzi hao, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Prof. Mohamed Janabi alisema kuwa hali ya mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yanayoendelea nchini Sudani imesababisha kufungwa kwa vyuo na baadhi ya shughuli kusimama hivyo watalamu hao kushindwa kuendelea na ratiba yao ya masomo ya kawaida.

"Wanafunzi hawa wapo mwaka wa tano wa shahada ya kwanza ya utabibu, ambapo katika mwaka huo, mafunzo hufanyika kwa vitendo zaidi, hivyo madaktari hawa wanafunzi watafanya mzunguko (Rotation) katika idara mbalimbali ikiwemo idara ya upasuaji chini ya usimamizi wa madaktari bingwa ili kuhakikisha wanapata maarifa yanayotakiwa" alisema Prof. Janabi

Alibainisha kuwa MNH itatoa fursa kwa wataalamu hao kujifunza kama ambavyo inatoa kwa wataalamu wengine wa ndani na nje ya nchi na hata baada ya kumaliza masomo kama watapenda kufanya mafunzo tarajali (Intenship) MNH itawapa nafasi hiyo.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa chuo cha UMST, Prof. Mamoun Homeida alisema kuwa amefurahi kuona wanafunzi kutoka chuo anachokisimamia wamepokelewa vizuri na kwamba jambo hili limetokana na mahusiano ya kindugu yaliyopo baina na Tanzania na Sudan.

Kwa upande wake Bi. Ruba Anwar Salih ambaye ni kiongozi wa kundi la wanafunzi hao alisema kuwa wamefurahi kupata fursa ya kuendelea na masomo katika Hospitali kubwa na yenye wataalamu wa kutosha, ni imani yao kwamba watapata fursa nzuri ya kujifunza.



# Msivilazimishe vituo kununua dawa kwa washitiri mnaowataka.

Na Rayson Mwaisemba
Dodoma.

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel ametoa wito kwa Wasimamizi wa Afya ngazi ya Mkoa kuacha tabia ya kuvilazimisha Vituo vya kutolea Huduma za Afya kununua dawa kwa washitiri ambao wanawataka wao ili kutatua kero ya uhaba wa dawa katika vituo pindi washitiri hao wanapokuwa na upungufu wa dawa.

Dkt. Mollel alisema hayo leo Juni 20, 2023 wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu Mhe. Asia Abdukarimu Halamga katika Bunge la kumi na mbili, Mkutano wa kumi na moja kikao cha 51, Jijini Dodoma.
Amesema, kuna baadhi ya Mikoa wameweka mshitiri (Prime Vendor) mmoja na huku kutoruhusu wataalamu katika vituo kununua dawa nje ya huyo mshitiri, kwahiyo anapokuwa amekosa bidhaa za dawa na vifaatiba kutoka Bohari Kuu ya Dawa au kwa huyo mshitiri, inasababisha kuwa na uhaba wa Dawa katika vituo hivyo.

Aidha, aliwaelekeza Viongozi wa Afya katika Mikoa kutengeneza biashara huria ili vituo viweze kununua dawa kwenye kwa mshitiri yoyote alietimiza vigezo ili kuondokana na changamoto ya uhaba wa dawa inayoweza kuepukika.

Sambamba na hilo Dkt. Mollel alisema, katika kuhakikisha dawa zinapatikana wakati wote kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, Serikali imeendelea kuiwezesha MSD mtaji ili iweze kufanya kazi kama Bohari ya dawa badala ya kufanya kazi kama Idara ya manunuzi.

Aliendelea kusema, Serikali imetoa kiasi cha shilingi Bilioni 16 kwaajili ya kutunza na kusambaza dawa kila mwezi, na kueleza kuendelea kusimamia muongozo wa matibabu katika kuhakikisha dawa zinazonunuliwa, kutunzwa na kuandikwa na madaktari zinazingatia muongozo wa matibabu.

Pia, alisisitiza kuwa, Wizara imeendelea kuboresha eneo la maoteo ya bidhaa za afya na kuchukua hatua kwa upungufu unaobainika, huku akisisitiza kuendelea kufunga mifumo ya kielektroniki ili kuimarisha usimamizi wa dawa na kuwezesha dawa kutolewa kulingana na wagonjwa husika.

# Zaidi ya Shilingi Bilioni 5.4 zimetengwa kwa ajili ya vifaatiba katika Hospitali ya Meta, Mbeya.



Na Rayson Mwaisemba
Arusha.

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amebainisha kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Afya ilitenga zaidi ya Bilioni 5.4 kwaajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika jengo la mama na mtoto META, katika hospitali ya Rufaa ya kanda nyanda za juu Kusini - Mbeya na tayari kupitia MSD vifaa hivyo vimepelekwa kwaajili ya usimikwaji.

Hayo yalisemwa leo Juni 12, 2023 wakati akijibu swali la Mbunge wa viti maalumu Mhe. Suma Ikenda Fyandomo katika Mkutano wa kumi na moja kikao cha kumi na mbili Mkutano wa 46, Jijini Dodoma.

Alisema, "katika mwaka wa fedha 2022/2023 serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 5.4 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya jengo la huduma za Mama na Mtoto katika Hospitali ya META ya Mkoa wa Mbeya."

Aliendelea kusema, jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya META limeanza kutumika na ufungaji wa vifaa tiba katika vitengo mbalimbali unaendelea na unatarajia kukamilika mapema Mwezi Julai 2023 ili wananchi wanaohitaji huduma za aina mbalimbali waendelee kunufaika na huduma hizo.

Aidha, Dkt. Mollel alisema, Serikali imeendelea kuboresha huduma katika vituo vyote vya utoaji huduma ikiwemo hospitali ya kanda ya KCMC huku zaidi ya Shilingi 983,612,500 hutumika kila mwezi kwaajili ya kulipa stahiki na mishahara ya watumishi 905 waliopo katika hospitali hiyo.

Pia, Dkt. Mollel alisema, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imepeleka kiasi cha shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya Dawa, vitendanishi na vifaa tiba ili kuwahudumia wananchi wanaofika kupata huduma katika hospitali ya KCMC, huku kiasi cha Shilingi bilioni 5.9 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya hospitali hiyo na shilingi milioni 263.6 kwa ajili ya uendeshaji.

Sambamba na hilo, Alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetoa ufadhili wa masomo ya ubingwa bobezi kwa watumishi 15 wa kada za afya wa KCMC wanaosoma ndani na nje ya nchi.

Kwa upande mwingine, Dkt. Mollel alisema Wizara ya afya kwa kushirikiana na Wizara ya fedha na OR Utumishi zinaendelea na mchakato ili kuhakikisha hospitali za Rufaa za kanda-Mbeya, pamoja na KCMC zinakuwa taasisi.

# Wananchi watakiwa kuzingatia mtindo bora wa maisha.

Na Majid Abdulkarim, Dodoma.

Serikali inaendelea kuwahimiza wananchi kuzingatia mtindo bora wa maisha kwenye lishe kwa kula chakula bora pamoja na kufanya mazoezi ya mara kwa mara ili kujiepusha na magonjwa yasiyo ya kuambikiza.

Ushauri huo ulitolewa na katibu Mkuu Wizara ya afya , Dk Seif Shekalaghe wakati wakati wa akifunga mafunzo kwa wataalamu wa afya juu ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza yaliyodumu kwa muda wa siku tano Jijini Dodoma.

Dkt. Shekalage alisema magonjwa ambayo sio ya kuambukiza yanaeletwa na mfumo wa maisha anayosihi mwanadaimu ikiwa ni pamoja na kutokufanya mazoezi.

“Hatufanyi mazoezi muda wote tupo ofisini, tukitoka hapo tunapanda gari tunaenda nyumbani, ukifika nyumbani unaangalia TV mpaka saa nne na wakati umekaa, chakula unaletewa hapo hapo unaenda kitandani unalala ukiamka asubuhi unapanda gari, unaenda kazini, hakuna mazoezi,”alieleza Dkt. Shekalage.

Aliongeza kuwa hata kutembea ni mazoezi wengine wanajua mazoezi lazima ukimbie au uende Gym hata kutembea ni mazoezi bila kusahau kuzingatia ulaji wa vyakula bora na sio bora kula tu.

“Ni muhimu sana ulaji wetu tuuangalie,vyakula ambavyo vinafaa sana ni mbogamboga nyingi,matunda pamoja na Wanga na tule kwa kiasi kuna wataalamu wanasema kula unapokuwa na njaa’, alisema Dkt. Shekalage
Kwa kuongezea amesema kuwa Ajali nazo kwa sasa ni magonjwa ambayo sio ya kuambukiza hivyo barabarani watu wawe makini.



# Kamati ya Bunge yampongeza Rais Dkt. Samia kwa kuboresha Sekta ya Afya.

Na Hassan Kimweri,
Dodoma.



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI imempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutumia fedha za UVIKO kuboresha Sekta ya afya ili wananchi kupata huduma bora.

Kauli hiyo ilitolewa leo jijini Dodoma na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile baada ya kufanya ziara katika Hospitali ya Taifa ya magonjwa ya afya ya akili Milembe na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma.



Dkt. Ndungulile alisema kuwa, zaidi ya Bilioni 10 zimetumika kuboresha Sekta ya Afya ambapo katika hospitali ya Hospitali ya Taifa ya magonjwa ya afya ya akili Milembe wameona jengo la kisasa la wagomjwa wa dharula, jengo la wagonjwa mahututi na mashine ya mionzi (X-RAY).

Katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma waliweza kutembelea jengo la wagonjwa wa dharura pamoja na jengo la wagonjwa mahututi na kuona Serikali ilivyoboresha maeneo hayo kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aidha, alitoa wito kwa Wizara ya afya kuongeza nguvu zaidi katika huduma za afya ya akili kwani hivi karibuni matatizo hayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi.

"Hivyo ili kuendana na kasi ya kuongezeka kwa matatizo ya afya ya akili nchini kuna haja ya ya kusogeza huduma za afya ya akili katika ngazi ya msingi ili kusaidia wananchi walipo katika maeneo ya kata, vijiji vyote katika majimbo yetu." Alisema Dkt. Ndungulile.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel alitoa rai kwa kamati hiyo kuwa na utamaduni wa kutembelea hospitali na taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara ya afya ili kushuhudia uwekezaji mkubwa uliofanyiwa na Serikali kwenye eneo la afya chini ya Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.



# Serikali yadhamiria kutokomeza Malaria hadi ifikapo 2030

Na Rayson Mwaisemba, Dodoma.

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amebainisha kuwa Serikali kupitia Mpango wa Taifa wa Malaria imepanga kutokomeza ugonjwa wa Malaria ifikapo mwaka 2030.

Dkt. Mollel alisema hayo Juni 23, 2023 wakati akijibu swali la Mbunge wa viti maalumu Mhe. Bernadetha Kasabago Mushashu katika kikao cha Bunge Jijini Dodoma.

Dkt. Mollel alisema mpaka sasa ni zaidi ya Mikoa 9 ambayo ugonjwa wa Malaria upo chini ya asilimia 1, hii ni kufuatia jitihada za Serikali kupitia Wizara ya Afya kutekeleza afua mbalimbali za kudhibiti maambukizi ya Ugonjwa huo ikiwemo unyunyiziaji ya viuadudu pamoja na matumizi ya vyandarua vyenye dawa.

Alisema, Serikali kupitia ya Wizara ya Afya imewasilisha maombi ya kiasi cha shilingi Bilioni 22 kwaajili ya kutekeleza afua za mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria nchi nzima, huku akisisitiza kuwa upo ushirikiano baina ya nchi ya Tanzania na nchi ya Rwanda katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria hasa katika Mikoa iliyo karibu na nchi hizo.

Aidha, Dkt. Mollel alisema Mkoa wa Kagera ni moja kati ya mikoa mitatu inayoongoza kuwa na ugonjwa wa Malaria nchini ukiwa na asilimia 18, huku Mikoa mingine ikiwa ni Tabora ikiwa na asilimia 23, na Mkoa wa Mtwara.

Sambamba na hilo, alisema katika kutokomeza kabisa ugonjwa wa Malaria Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kusambaza vyandarua vyenye dawa kwa jamii kupitia kampeni za kugawa vyandarua kwa kila kaya, kliniki za mama wajawazito na watoto na vituo vya kutolea huduma kwa makundi maalum kama wazee.

Unyunyiziaji wa viuadudu vya kibaiolojia kwenye mazalia unaendelea ili kuuwa viluilui wa mbu (Biolarviciding) katika maeneo yenye maambukizi ya Ugonjwa wa Malaria, alisisitiza Dkt. Mollel.

Pia, Dkt. Mollel alisema, Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea na utoaji wa elimu pamoja na kuhamasisha jamii kutumia njia mbalimbali za kujikinga na ugonjwa wa malaria ili kufikia lengo la kuutokomeza ugonjwa huo.



# Wadau wa maendeleo kushirikiana na Baraza kutokomeza Malaria nchini 2030.

Na Majid Abdulkarim
Dar Es Salaam.

Mwenyekiti wa Baraza la Kutokomeza Malaria Tanzania, Leodigar Tenga ametoa wito kwa wajumbe wa baraza kuwa karibu na wadau wa maendeleo wa afya kwa ajili ya kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2030.

Bw. Tenga alitoa rai hiyo leo katika ziara ya Baraza hilo walipotembelea kiwanda cha Viuadudu Kibaha Mkoani Pwani na kujionea shughuli zinazofanyika katika kiwanda hicho.

Tenga alisema ili kufanikisha kutokomeza malaria nchini jamii inapaswa ipatiwe elimu sahihi ya matumizi ya afua mbalimbali ikiwemo matumizi ya viuwadudu katika kuharibu mazalia ya mbu katika mazingira.

Aidha, Tenga alitoa Rai kwa Serikali kuhakikisha halmashauri zote nchini hususani zenye kiwango kikubwa cha Malaria kununua na kutumia viwadudu vinavyotengeneza katika kiwanda cha Tanzania Biotech Product Limited.

Kwa upande wake Mmoja wa Wajumbe wa Baraza hilo, Faraja Nyarandu alisema kuwa ziara hiyo imekuwa chachu kwao kwani amejifunza na kuona nafsi ya dawa katika vita vya kutokomeza malaria nchini.

Lakini pia alieleza kuwa kuna dawa zinatengenezwa hapa nchini ambazo zinaweza tumika kuharibu mazalia ya mbu na kufanya Tanzania kuwa salama juu ya malaria kwa kuua mazalia ya mbu kabla haja sambaza vimelea kwa mtu.

“Tumepata chachu ya kubuni mikakati itakayo saidia kujibu changamoto za sehemu husika katika vita dhidi ya malaria Tanzania ambapo tunaona maeneo yenye kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria afua zake haziwezi kuwa sawa na maeneo yaliyonakiwango cha chini “. Alisisitiza Nyarandu.

Vile vile, alielezea kuwa wamepata elimu juu ya kudhibiti wa mazalia ya mbu huku akiitaka jamii kuchukua tahadhari dhidi ya malaria kwa kutumia chandarua na kupima ili kujua afya.




# Mfumo wa M- Mama wazinduliwa Hospitali ya Sekoutoure, Mwanza

Na Mwandishi wetu
Mwanza.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza Ndg.Balandya Elikana amezindua rasmi mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa wakina mama wajawazito waliojifungua na watoto wachanga (m-mama) na kuwataka wahusika wote na mfumo huo kutekeleza wajibu wao kwa weledi.

Akizungumza na wafanyakazi wa kitengo hicho kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza, Sekou Toure, Balandya alisema lengo la kuanzishwa kwa mfumo huo ni kuepuka vifo vya mama na mtoto ambapo Mkoa wa Mwanza unakabiliwa na Changamoto hiyo, hivyo haitakuwa na maana kama wahusika wataonesha kuzembea katika kuteleza wajibu wao ipasavyo.

"Serikali ya Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeipa kipaumbele Sekta ya afya kwa kuboresha maeneo mbalimbali likiwemo hili la mfumo ambao ulizinduliwa na Rais wetu," alisema Mtendaji huyo wa Mkoa.

Aliongeza kuwa wahusika wote wa kada ya afya sasa watambue ni wajibu wao kuja na matokeo yenye tija wakati Serikali ikiweka mikakati mbalimbali ya kuwaboreshea huduma wananchi wake.

"Mimi nikiwa Muuguzi Mkuu wa Mkoa, nimeguswa kwa namna ya pekee na huduma hii kwani ni yenye nia njema kwa wakina mama na watoto na hasa kwa wale walio katika maeneo yenye changamoto ya umbali na usafiri,"Bi. Claudia Kaluli, Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa.

Nae Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza, Dr. Bahati Msaki alisema kuwa "Kazi yetu ni kuhakikisha wagonjwa wanapata huduma bora bila kuchelewa hususani mama na mtoto"

Afisa mwandamizi wa TEHAMA kutoka Wizara ya Afya, Jackson Shayo alisema mfumo huu umeonesha kuitikiwa vyema Bara na Visiwani hali ambayo inaonesha ni mkombozi kwa wakina mama wajawazito na wototo.

Huduma hiyo ya m-mama ilifanikishwa na baadhi ya marafiki wa Maendeleo ikiwemo Vodafone Foundation, Pathfinder International na Touch Foundation Jumla ya madereva 114 wameingia mkataba wa kutoka huduma hiyo katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Mwanza

# MOI watoa mafuzo kwa wataalam katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga



Na Mwandishi wetu
Shinyanga.

TAASISI ya Mifupa Muhimbili (MOI) imeanza kutoa mafunzo kwa Madaktari wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga wa Idara ya Magonjwa ya ndani (Internal Medicine), ili kuwajengea uwezo zaidi wa kutoa huduma za Afya.

Mafunzo haya yalianza rasmi Jumatatu ya Juni 26, 2023, yaliwezeshwa na Dkt. Hamis Shaffih Hamis pamoja na Muuguzi Dorcas Gideon Magawa (wote kutoka MOI), ambayo yalidumu kwa muda wa wiki moja hadi Juni 30, 2023.
Akizungumza wakati wa mafunzo, Muuguzi Magawa alisema lengo mama la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo Watumishi wa Afya katika kuboresha kazi na kutoa huduma bora kwa za Afya kwa wagonjwa.
“Lengo kuwa la kutoa mafunzo haya ni kuhakikisha tunawajengea uwezo Madaktari ili waweze kuimarika vema katika utoaji wa huduma bora za Afya.
“Mafunzo haya yamelenga zaidi katika kutoa huduma za dharura kwa wagonjwa, hivyo tumekuja kutoa elimu zaidi ya nadharia na vitendo ili kuhakikisha huduma bora zinapatikana katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga”, alisema Magawa.
Aidha, Magawa aliwaomba Madaktari waliopata mafunzo hayo kuwa ni vema mafunzo haya yakaendelezwe kwa kuwasaidia Wataalamu wengine wa Afya kwa kuwafundisha ili kuhakikisha kunakuwa na wigo mpana wa huduma za Afya utakaosaidia kuongeza wingi wa wataalamu.
Katika kuboresha huduma za Afya na kuongeza uwezo kwa wataalamu, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga iliendelea na utaratibu wake wa kawaida wa kuhakikisha inawejengea uwezo zaidi Madaktari wake kwa kuitisha mafunzo haya ili kukuza wigo na kutoa huduma bora za Afya kwa wananchi.

# Upasuaji wa kwanza wa ukarabati wa mrija wa mkojo wafanyika Hospitali ya Ligula Mtwara.




Na Mwandishi wetu, Mtwara.

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara(LIGULA) kwa kushirikiana na Madaktari Bingwa wa Mama Samia kwa mara ya Kwanza Wamefanya Upasuaji wa Ukarabati wa Mrija wa Mkojo(Urethroplasty ) kwa Kuchukua Nyama sehemu ya Mdomo wa Mgonjwa na Kuipandikiza kwenye Sehemu ya Mrija wa Mkojo wa Mgonjwa ambae alionekana na Shida ya kuziba kwa Mrija wa Mkojo baada ya Uchunguzi wa Mionzi Kutoka Kambi Maalumu ya Madaktari Bingwa Wa Mama Samia kufanyika.

Akizungumza baada ya kukamilisha Upasuaji Dkt Hussein Msuma (Daktari Bingwa Bobezi wa Upasuaji wa Mfumo wa mkojo nchini) alisema Upasuaji huo ulimpunguzia Gharama kubwa Mgonjwa huyo baada ya kuudhuria katika Kambi Maalumu ya Uboreshaji wa Huduma za Afya nchini, Kambi ya Madaktari Bingwa wa Mama Samia.

Sambamba na hilo Daktari huyo Bingwa Bobezi wa Mfumo wa mkojo aliwajengea uwezo Madaktari wa ndani wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara (LIGULA) Kuwahudumia Wagonjwa wenye Matatizo ya Mfumo wa Mkojo kuanzia hatua ya kuwaona katika kliniki za Upasuaji hadi Kuwafanyia Upasuaji.




Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Iringa Dkt.Alfred Mwakalebela amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh.Dkt Samia Suluhu Hassa kwa kuipatia Hospitali kiasi cha shilingi bilion 3.8 kwaajili ya uboreshaji wa miundo mbinu na vifaa tiba ili kuwasaidia wananchi.

Alisema kuwa katika kipindi cha miaka 2 ya Rais Hospitali hiyo imeweza kujenga jengo la CT SCAN pamoja na kutoa huduma hiyo ambayo imekuwa msaada mkubwa kwa wananchi na kuwapunguzia gharama na muda wa kwenda umbali mrefu kufuata huduma hiyo



# Serikali yatoa Bilioni 7.3 ujenzi wa majengo ya kutolea huduma za upasuaji, Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Mbeya

Na Mwandishi wetu
Mbeya.

Katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi, Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Mbeya inafanya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Jengo la upasuaji la kisasa na wodi zake, Serikali kupitia Wizara ya Afya, imetoa kiasi cha shilingi Bilion 7.3 kwaajili ya ujenzi wa jengo la la upasuaji, wodi za upasuasi na mifumo ya hewa tiba.

Mradi huo mpaka sasa umegharimu shilingi Bilioni saba milioni miatatu sabini na saba laki tatu themanini na nane miamoja na tatu na senti sitini na mbili, Ambapo utekelezaji wake ulianza mwezi Julai, 2020 hadi sasa mradi umekamilika kwa asilimia 99%. Hii ni kutokana na kazi nzuri inayoendelea kufanywa na Serikali ya awamu ya sita chini ya usimamimizi wa Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kupitia wizara ya Afya.

Ujenzi wa jengo la upasuaji lenye vyumba vya upasuaji (theater) sita na wodi zenye uwezo wa kuhudumia wagonjwa kwa wakati mmoja themanini na tisa (89), aidha wagonjwa sita (6) wataweza kufanyiwa upasuaji kwa wakati mmoja. Hivyo mra di huu utasaidia kuongeza uwezo wa hospitali kutoa huduma bora na za kisasa za upasuaji kwa wananchi wa mkoa wa Mbeya na maeneo ya jirani bila ya kuwalazimu kufuata huduma hiyo mbali na eneo lao.





TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA • AFYA NI MTAJI

**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI JUNI, 2023**